

* KKKT wazindua mradi wa ng'ombe >

Kahama. Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa kushirikiana na Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria wamezindua mradi wa kupandisha ng'ombe wa nyama na maziwa kwa njia ya mrija kwa wafugaji 97 wa Halmashauri hiyo. Msaidizi wa askofu wa dayosisi hiyo, Yohana Nzeli alisema mradi huo utasaidia kuondokana na uzalishaji wa ndama dume na kupata majike na ongezeko la maziwa ya kutosha kwenye kaya za wafugaji hao. **(Shaban Njia)**



* Wanaotelekeza wazee kukiona

Shinyanga. Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk Philemon Sengati ameahidi kulifanyia kazi suala la wazee wanaotelekezwa na watoto wao. Alitoa ahadi hiyo jana, baada ya baadhi ya wazee kudai kutelekezwa na watoto wao na wengine kuachiwa kulea wajukuu. Sengati alikuwa katika kikao cha pamoja na wazee wa Mkoa wa Shinyanga, ikiwa ni hatua yake muhimu ya kukutana na kusikiliza makundi tofauti ya jamii. **(Mwandishi Wetu)**